



THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

SCHOOL BASED ASSESSMENT

KISWAHILI SEHEMU B na C

For

Regular Learners

And Learners with

Physical Impairment

Gredi ya 8

Septemba/Oktoba 2026

Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa

JINA LA MWANAFUNZI_____

GREDI _____

TAREHE_____

MUDA: SAA 2

KWA MATUMIZI YA MTAHINI

JEDWALI LA ALAMA

SEHEMU YA B												
SWALI	ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA								ZOEZI 4: UFUPISHO			
SWALI	1	2	3	4	5	6	7	8	9	10	11	12
UPEO	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1	1
ALAMA												

	ZOEZI 5: SARUFI												
SWALI	13	14	15	16	17	18	19	20	21	22	23	24	25
UPEO	1	1	1	1	1	1	2	2	2	2	2	2	2
ALAMA													

	ZOEZI 6: KUANDIKA
SWALI	26
UPEO	4 - Kiwango cha juu cha kutathminia (Performance Level)
ALAMA	

SEHEMU YA C		
ZOEZI 7: FASIHI		
SWALI	27	28
	FASIHI SIMULIZI	TAMTHILIA
UPEO	10	10
ALAMA		

SEHEMU YA B

ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 4.

Maliasili ni jumla ya vitu vya kimaumbile vinavyopatikana katika nchi. Nchi yetu imetunukiwa maliasili za aina nyingi. Kuna misitu yenye miti ya aina mbalimbali kama vile mikalatusi, mivule na mibuyu. Licha ya kuwa kivutio cha mvua, miti pia husafisha hewa na kutupatia dawa za kiasili. Mandhari ya kijiografia ya nchi hii hupendeza mno. Ukitembea nchini utaona milima, mabonde na hata nyika zenye mvuto mkuu. Kadhalika kuna mito, maziwa na bahari ambazo ni hifadhi ya samaki na viumbe wengine wa majini.

Wanyama wa porini pia ni maliasili muhimu nchini. Wao huvutia watalii ambao huja kuwaona wanyama kama vile tembo, simba, mbogo, duma na hata sokwe. Ada wanazolipa watalii hao huiletea nchi yetu fedha za kigeni. Nchi yetu pia ina madini ambayo **huupiga jeki uchumi**. Makaa, soda na hata dhahabu ni baadhi ya madini hayo. Madini haya hutumiwa kama malighafi kutengenezea bidhaa mbalimbali viwandani.

Ipo haja ya kuitunza maliasili za nchi. Ukataji miti ovyo unafaa kukomeshwa. Ni jukumu la kila mwanajamii kujifunga mkaja kupanda miti ya aina mbalimbali ili kuendelea kukuza misitu. **Mmomonyoko wa udongo unafaa kudhibitiwa ili kudumisha ardhi yenye rutuba kwa ukulima.** Wanyama wa porini nao hawana budi kulindwa dhidi ya mauaji ya kiholela yanayotekelezwa na wasasi haramu. Maeneo ya mito yanastahili kuhifadhiwa wala yasigeuzwe kuwa makazi. Mwisho, utafiti unafaa kufanywa ili kugundua maliasili ambazo huenda zinapatikana nchini ili ziweze kutumiwa kwa njia endelevu.

1. Mbali na kusafisha hewa, miti pia

2. Kwa mujibu wa kifungu nchi yetu itapata hasara gani tusipotunza maliasili?

3. Kauli ‘**Mmomonyoko wa udongo unafaa kudhibitiwa ili kudumisha ardhi yenye rutuba kwa ukulima**’ imetumiwa kwenye kifungu. Unadhani ni njia ipi jamii itatumia ili kuzuia mmomonyoko wa udongo?

4. Nahau, ‘**huupiga jeki uchumi**’ imetumiwa kwenye kifungu kumaanisha:

Geuza ukurasa

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 5 hadi la 8.

Ukuaji na kudumu kwa jamii yoyote ile kunategemea watoto. Wao ndio wanaorithishwa thamani na amali za jamii ili kuzitunza na kuzipokeza kwa vizazi vingine. Zipo haki za kimsingi ambazo sharti watoto hawa wahakikishiwe ili kutekeleza jukumu hilo.

Haki ya kimsingi zaidi kwa mtoto ni chakula cha kutosha na chenye lishe bora. Chakula hicho kiwe na virutubisho vya wanga, protini na vitamini. Aidha, mtoto ana haki ya kuishi katika makazi salama; yawe na mahali pazuri pa kulala, hewa safi na joto ili watoto wapate pumziko la kutosha baada ya shughuli nyingi za siku.

Katiba ya nchi inamhakikishia kila mtoto elimu bora ya msingi bila malipo. Ni **hatia** kwa mzazi au mlezi yeyote kumnyima mtoto nafasi ya kujiunga na shule na kukamilisha elimu ya msingi. Isitoshe, watoto wanastahili kuwa na afya bora. Wanapougua hawana budi kutafutiwa huduma zifaazo za matibabu.

Jamii ina wajibu wa kuhakikisha kuwa haki za watoto zimelindwa. Wanaoendeleza dhuluma dhidi ya watoto wachukuliwe hatua kali. Watoto nao waelimishwe kuhusu nafasi yao katika kujihakikishia haki.

5. Kwa nini jamii inawategemea watoto? _____

6. Ni jibu lipi sahihi kulingana na kifungu?

- A. Chakula kikitosha, virutubisho huongezeka mwilini mwa mtoto.
- B. Mtoto anayefanya shughuli nyingi hulala mahali salama.
- C. Jamii imeweka mikakati ifaayo kumhakikishia mtoto elimu.
- D. Afya ya mtoto ikiimarika atafahamu haki zake.

7. Unadhani wanaowadhulumu watoto watachukuliwa hatua gani?

8. Kisawe cha neno **hatia** ni: _____

ZOEZI 4: UFUPISHO

Soma kifungu hiki kisha ujibu swali la 9 hadi 12.

Siku hizi kuna njia anuwai za kuwasiliana. Njia mojawapo na ambayo imewateka watu wengi ni mitandao ya kijamii. Njia hii ya mawasiliano inatoa fursa kwa watu kote ulimwenguni kupashana habari kuhusu masuala na matukio mbalimbali yanayoathiri jamii. Kuwasiliana kwa njia ya mtandao pia huwezesha kubadilishana mawazo, kuendeleza biashara, kujifunza na hata kufanya kazi za kujipatia riziki. **Hata hivyo, mitandao hii imejaa visa vya uhalifu ambavyo vinatishia kusambaratisha mahusiano na mshikamano wa kitaifa na kimataifa.**

Uhalifu wa mitandaoni unarejelea shughuli zozote haramu zinazoendelezwa na watu wenye nia potofu kwenye mitandao. Shughuli hizi za kihalifu ni nyingi. Kuna watu ambao huwalaghai watumiaji wa mitandao na kuwaibia mali zao. **Wengine huwasababishia wenzao dhiki za kisaikolojia kupitia kwa mfano, kuwarejelea kwa majina au maneno ya kuwaaibisha, kuwahusisha na habari za uongo na kutoa habari zao za kibinafsi. Isitoshe, mitandaoni watu wengine huchukua utambulisho wa wenzao na kufanya uhalifu kisha kuwatia wenzao matatani au hata kufaidika kwa njia haramu.**

Ili kupata manufaa yafaayo ya mitandao, ipo haja ya kuwa makini wakati wote tunapoendelea shughuli humo. Tutumie nywila imara au madhubuti kila wakati tunapofungua kumbi zetu. Tunastahili pia kuepuka kusakura kwenye tovuti au viungo visivyoaminika. Aidha, ni sharti tuepuke kutangamana na watu tusiowafahamu. Ikitokea kwamba tunawashuku watu hawa, tunastahili kupiga ripoti ama kwa walezi wetu au kwa vituo vya usalama. Kimsingi, watumiaji wa mitandao wanafaa kuzingatia kanuni za kimaadili kila mara wanapotumia mitandao ili wawe salama.

9. Eleza manufaa ya mitandao kwa maneno **12**.

10. Andika methali inayojumuisha ujumbe wa kauli iliyokolezwa rangi katika aya ya **kwanza**.

11. Fupisha ujumbe wa kauli zilizokolezwa rangi katika aya ya **pili** kwa maneno **15**.

12. “Kukomesha uhalifu ni jukumu la mtu binafsi.” Thibitisha kauli hii kwa kutumia maneno **25** ukirejelea aya ya **mwisho**.

Geuza ukurasa

ZOEZI 5: SARUFI

Kasimo 13 kwa Kato jioni hiyo alipokelewa sebuleni kisha 14 mazungumzo baina 15 . Kasimo alimkumbusha kuwa 16 aliohitaji kuanzisha mradi wa kufuga ng'ombe 17 tayari.

- | | | | |
|-------------------|---------------|--------------|----------------|
| 13. A. alipofikia | B. alipofikwa | C. alipofika | D. alipofikiwa |
| 14. A. wakaanza | B. wakianza | C. wangeanza | D. wanaanza |
| 15. A. yenu | B. yake | C. yetu | D. yao |
| 16. A. riba | B. mtaji | C. kodi | D. bima |
| 17. A. ilikuwa | B. ulikuwa | C. lilikuwa | D. kulikuwa |

18. Sentensi ifuatayo ina viwakilishi. Tambua kiwakilishi cha idadi. (alama 1)

Hawa wametengeneza vichache sana.

19. Akifisha sentensi ifuatayo: (alama 2)

Salaala meli hiyo imengoa nanga na mizigo hiyo yote

20. Jaza nafasi kwenye sentensi ifuatayo kwa viambishi sahihi. (alama 2)

Ulezi mwema__ nahimizwa ili kukabiliana na maovu__ liyojaa ulimwenguni humu.

21. Andika sentensi zifuatazo upya kwa kufuata maagizo:

- i. Kombo alifuma fulana yake kwa uzi imara. (Hali ya mazoea) (alama 1)
-

- ii. Ndizi za mtoto wangu zimepikwa vizuri. (Hali ya udogo) (alama 1)
-

22. Kinyume cha neno **juu** ni **chini**. Tunga sentensi ukitumia kinyume cha neno **tenganisha**. (alama 2)
-

23. Kanusha sentensi ifuatayo : (alama 2)

Julita na Paulo wamewasaidia mayatima .

24. Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi. (alama 2)

[illegible]

7

[illegible]

SEHEMU YA C: (alama 20)

ZOEZI 7: FASIHI

27. *Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali.*

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali.

Mwanzoni mwa ulimwengu, hakukuwa na mja yeyote duniani. Mulungu, yaani Mwenyezi Mungu, ndiye aliyewafinyanga binadamu wa kwanza wa jamii ya Wakamba kwa viganja vyake viwili. Hakuwafinyanga kwa udongo kama chungu! La, hasha. Waulize wahenga, nao watakwambia kuwa awali **Mulungu alimuumba mwanamume kutoka kule-e-e mbinguni**. Kisha akamuambia mkewe, kipusa wa kuonewa kijicho na viumbe wote, huko huko mbinguni. Aliwaweka wawili hawa kwenye jabali la Nzau. Hayo ndiyo makazi aliyowajalia Mulungu kwa aushi yao yote. Hapo ndipo alama za nyayo zao na za mifugo wao zinapopatikana hadi sasa.

Mulungu aliwabariki waja hawa kwa mengi. Si mifugo, si mashamba yaliyosheheni mavuno msimu hata msimu, si mawe ya thamani.... Vyote hivi viliwazunguka kana kwamba vinawaabudu. Siku zilivyozidi kusonga, ndivyo milango ya heri ilivyozidi kuwanyooshea mikono. Mulungu alimfungulia kizazi yule kipusa, akakipakata kilaika, kifunguamimba. Nacho kilikuwa kivulana; chenye sura jamali na uso ulioonyesha upole wa malaika. Hiki kilifuatwa na vijogoo vingine, nadhani vilikuwa tisa! Mume na mke wakawa vinywa wazi, wakatazana hivi kana kwamba wanaulizana watafanikiwa vipi kutekeleza amri ya Mulungu ya kuujaza ulimwengu. Hata wewe ungejiuliza hivyo hivyo.

Wakiwa katika hali hiyo, Mulungu alianguka mvua kubwa kutoka huko juu *Ituni* alikoishi, nayo ilinyesha kidindia kwa wiki mbili, ikaicharaza ardhi, ikaicharaza ardhi, hadi ardhi yenyewe ikaanza kulalamika. Hata mvua ilipoanza kupusa, viumbe wengine wawili, mwanamume na mwanamke walitokea kwenye vichuguu vilivyojaa furifuri kwenye eneo hilo. Ajabu iliyoje! Ni kana kwamba Mulungu alisikiliza sala za yule bwana wa jabali au tuseme ile familia ya mbinguni. Binadamu hawa wa kichuguu walijaliwa watoto wa kike, mabarobaro wa ile familia ya mbinguni wakashusha pumzi, wakawa wamepata majiko. Usidhani walipewa mabinti hawa bure! Wavyele wao waliipelekea familia ya Kichuguu maelfu kwa maelfu ya mifugo kama mahari, ikawa imepata utajiri isioulalia wala kuuamkia. **Naye binadamu ni nani?** Bwana na bibi wa Kichuguu waligeuka mkono wa birika, wakakataa katakata kumshukuru Mulungu. Hata kafara ya mbuzi aliyelemaa mguu walishindwa kutoa. Bila shaka unaweza kukisia matokeo ya haya.

Mulungu alijawa na ghadhabu inayoweza kumtia mja kifafa. Aliamua kuuwahi udongo uli maji. Alisababisha ukame ambao haujawahi kuonekana katika ulimwengu mzima. Eneo zima waliloishi binadamu hawa likapambwa kwa mizoga ya mifugo. Janga la njaa liliwakodolea macho, wakaona ku moto, wakaamua kutorokea kokote, bora watafute chakula wazisalimishe roho zao. Hii ikawa asili ya kutawanyika kwa jamii ya Wakamba kote ulimwenguni. Hata sijui walijizika wapi. Lakini, babu yangu alipokuwa akitusimulia hadithi hii alitambua kuwa baadhi ndio waliogeuka kuwa Wakikuyu, wengine Wameru na wengine kubakia kuwa jamii asilia ya Wakamba.

Geuza ukurasa

- a) Hiki ni kisasili. Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano **miwili** kutoka kwenye hadithi.
(alama 2)

- b) Eleza mafunzo **mawili** ambayo unapata kutoka kwenye familia ya Kichuguu.
(alama 2)

- c) Ili kufanikisha uwasilishaji wa hadithi, fanani huweza kutoa maoni yake kuhusu mhusika au jambo ambalo anahadithia. Toa mfano mmoja kutoka kwenye hadithi hii kuthibitisha matumizi ya mbinu hii ya uwasilishaji. (alama 1)

- d) Fikiria kwamba wewe ndiye fanani wa hadithi hii, je, utawasilishaje kauli iliyoandikwa kwa herufi nzito katika **aya ya kwanza?** (alama 2)

- e) Kauli, ‘ **Naye binadamu ni nani?**’ Ni swali la balagha. Swali hili lina umuhimu gani katika uwasilishaji wa hadithi hii? (alama 1)

- f) Eleza mbinu nyingine **mbili za lugha** ambazo zimetumiwa kufanikisha uwasilishaji wa hadithi hii. (alama 2)

28. TAMTHILIA

Soma sehemu ifuatayo ya tamthilia kisha ujibu maswali.

SEHEMU YA KWANZA

ONYESHO LA PILI

(Ni jioni, Nyumbani mwa Bwana Maarifa. Maarifa na mkewe Pendo wanashiriki chajio. Kimya kimetanda. Sauti pekee inayosikika ni ya vijiko vinavyokwaruzana na sahani mara kwa mara.)

Bwana Maarifa: *(Akipasua kimya.)* Mke wangu, kuna jambo ambalo nimekuwa nikiliwazia kwa muda sasa.

Pendo: *(Akimwangalia kwa makini.)* Lipi hilo mume wangu?

Bwana Maarifa: *(Akijikohoza.)* Mke wangu, kama unavyofahamu kazi yangu katika kampuni ya kutengeneza vigae ilikatika ka! Huu ni mwezi wa pili sasa.

Pendo: *(Akimpa motisha kuendelea.)* Enhee!

Bwana Maarifa: Hivi majuzi nilipokea ujumbe kutoka kwa benki ukiniarifu kuwa nimelipwa marupurupu ya kustaafishwa.

Pendo: *(Akitabasamu.)* Ahaa! Hiyo ni habari nzuri mume wangu. Gharama ya mahitaji huku nyumbani ilikuwa inaelekea kunibwaga chini. Hata sijawatembelea wavyele wangu kijijini. Huu mwaka wa pili sasa. Sasa nitapata angaa masurufu ya safarini.

Bwana Maarifa: *(Akibadilisha mkondo wa mazungumzo.)* Bila shaka huu ni wakati mzuri wa kupanga namna ya kutumia hela hizo kwani haya ndiyo malipo rasmi ya mwisho.

Pendo: *(Akionyesha haya.)* Ninakuunga mkono mume wangu. Katika mpango huo, usisahau kwamba hivi karibuni tutampokea mwanambee, inshaallah!

Bwana Maarifa: *(Akitabasamu.)* Hilo nalifahamu. Mke wangu, nimekuwa nikiwazia kuhusu mradi wa kufuga kuku. Unavyoona, tulibahatika kukinunua kipande hiki cha ardhi tunamoishi. Si kikubwa lakini kina nafasi ya kutosha kwa mradi huo.

Pendo: *(Akionekana mwenye mawazo.)* Tutayaweza mujukumu ya kuwatunza kuku? Je, tutamudu gharama ya kuwalisha na matibabu yao?

Bwana Maarifa: *(Akishusha pumzi.)* Mke wangu, usitie shaka kuhusu jukumu la kuendesha mradi huo. Nilivyokwisha kukufahamisha, sina kazi nyingine ya kufanya. Isitoshe, kuku wana manufaa mengi. Mayai na nyama yao ni chakula muhimu kwa binadamu. Tutafaidi lishe hiyo na pia kuuza ziada ili tupate hela. Kadhalika, mbolea ya kuku ina virutubishi muhimu kwa mimea. Hiyo itatumika kule shambani tunamokuza mboga.

Geuza ukurasa

Pendo: (*Akitikisa kichwa kukubaliana naye.*) Sasa nimekuelewa mume wangu. Pia, ninakushauri umtembelee Bi. Rasiberi ili ujifunze zaidi kuhusu mradi huo. Bi. Rasiberi ni mfugaji maarufu katika mtaa huu. Juzi, alinunua gari aina ya *pick-up* kwa ajili ya kuuendeleza mradi huo.

Bwana Maarifa: (*Akitabasamu.*) Naam, nitatafuta maarifa zaidi kabla ya kuanzisha. (*Kimya kidogo.*) Mke wangu, nilikuwa nimeweka akiba kidogo. Hiyo itagharamia safari yako ya kuwatembelea wazazi. Ni muhimu kufanya hivyo. Utakapokuwa tayari utaniarifu.

Pendo: Asante mume wangu. Tutashirikiana kufanikisha mradi huo.

(*Pendo anaondoa vyombo mezani.*)

(*Taa zinazimika.*)

- a) Bainisha sifa **mbili** za tamthilia zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

- b) Eleza maudhui **matatu** yanayojitokeza katika sehemu hii ya tamthilia. (alama 3)

- c) Fafanua sifa **tatu** za Pendo kwa mujibu wa onyesho hili. (alama 3)

- d) Toa mifano ya mbinu zifuatazo za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)

i. Tashihisi _____

ii. Nahau _____

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.